JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# KITINI CHA WAWEZESHAJI KUHUSU MAJADILIANO YA MILA NA DESTURI KATIKA JAMII

AGOSTI, 2023

DODOMA

## YALIYOMO

**YALIYOMO ........................................................... i**

**DIBAJI.............................................................. iv**

**SURAYA KWANZA: UTANGULIZI.......................... 1**

Usuli.......................................................... 1

MalengoyaKitini ............................................ 2

MatumiziyaKitini............................................ 2

WawezeshajiwaMajadiliano ............................ 2

**SURA YA PILI: MWONGOZO WA TAIFA WA UENDESHAJIMAJADILIANOKUHUSIANANA MILA NA DESTURI ZENYE MADHARA KWA JAMIIWAMWAKA2022 ........................................... 4**

RejeayaMwezeshaji...................................... 8

UmuhimuwaMwongozo .................................. 8

MadhumuniyaMwongozo............................... 9

MatumiziyaMwongozo .................................. 9

MilanaDesturiAmbazoMwongozo UnalengaKuzitokomeza/Kukabiliana............. 10

MpangiliowaMwongozo ............................... 11

SURAYATATU:USHIRIKISHWAJIWAJAMII ........... 12

TaarifazaMwezeshaji.................................... 16

Ushirikishwajijamii........................................ 16

FaidazaKushirikishaJamii............................ 17

AtharizaKutoshirikishaJamii......................... 18

MjadalaKatikaJamii ...................................... 18

**SURA YA NNE: KUENDESHA MAJADILIANO YA MILANADESTURINGAZIYAJAMII ........................... 20**

Kupangamajadilianongaziyajamii................ 20

TaratibuzaKuzingatiaKablaya Majadiliano20

Kuwezeshamajadilianokwenyejamii ............ 22

Mpangokazishirikishi ................................... 48

**SURA YA TANO: UFUATILIAJI NA TATHMINI SHIRIKISHI ........................................................ 51**

UfuatiliajiShirikishi........................................ 51

TathminiShirikishi ........................................ 52

UmuhimuwaKufanyaTathmini...................... 53

HatuazaTathminiShirikishi ........................... 53

## VIFUPISHO


| | |
|---|---|
| CBOs | Community Based Organizations (Mashirika ya Kijamii) |
| CDC | CentersforDiseaseControl |
| CDF | Children'sDiginityForum(Jukwaa la Utu wa Watoto) |
| CFTSW | Community Focus on Teen and Single Mothers Welfare |
| FBOs | Faith Based Organizations (Mashirika ya Kidini) |
| HACOCA | HurumaAIDSConcernandCare |
| MTAKUWWA | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto |
| NGOs | Non-Governmental Organizations (Mashirika Yasiyo ya Kiserikali) |
| TGNP | Tanzania Gender Network Programme (Mtandao wa Jinsia Tanzania) |
| UMTUU | Uhusano na Mlengwa, Tupio la tatizo, Ugunduzi binafsi na Utekelezajiwamaamuzi |
| UNFPA | United Nation Population Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa LinaloshughulikiaIdadiyaWatu) |
| UZIKWASA | UzimakwaSanaa |
| WiLDAF | Women in Law and Development in Africa(WanawakekatikaSheriana MaendeleoAfrika) |
| WMJJWMM | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |

## DIBAJI

Mila na Desturi ni muhimu katika maisha ya kila siku ya jamii yoyote ile, hususan zikitumika kwa Maendeleo na Ustawi wa Jamii husika. Katika jamii zetu zipo Mila na Desturi chanya zinazotokomeza ukatili zinazopaswa kuendelezwa na hasi zinazochochea ukatili zinazopaswa kutokomezwa. Baadhi ya Mila na Desturi zinachochea ukatili wa wanawake na watoto ni pamoja na ukeketaji, ndoazautotoni,utakasaji wa wanawakepamojana watoto wa kike kutoruhusiwa kurithi mali katika jamii. Upo umuhimu wa kufanya mageuzi ya kifikra namitazamo kupitia mijadala ngazi ya jamii Ili kuwezesha jamii kujadili na kukubaliana Mila na Desturi chanya za kuendelezwa na hasi za kutokomezwa.

Kwa kuzingatia hilo, Wizara imeandaa Kitini cha Wawezeshaji Kuhusu Majadiliano ya Mila na Desturi Katika Jamii cha mwaka, 2023 kwa ajili ya kuwezesha majadiliano ngazi ya jamii. Kitini hiki ni utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji wa Majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi zenye madhara kwa Jamii wa Mwaka 2022, ambao uliandaliwa kwa ajili ya kutekeleza sehemu ya pili ya Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto wa Mwaka 2016/17 hadi 2021/22.Mpango huo umefanyiwa mapitio ambapo umeandaliwa Mpango wa Pili unaotekelezwakuanzia mwaka 2023/24 hadi 2027/28.

Maandalizi ya Kitini yamehusisha wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi toka Wizara za Kisekta, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), Mashirika ya Kidini (FBOs), Mashirika ya Kijamii (CBOs) wanawake na watoto ambao pia ni walengwa wa utumiaji wa kitini. Wizara inatoa wito kwa watumiaji wa kitini hiki, kuhakikisha ushiriki kamilifu wa makundi yote ya jamii katika mijadala husika. Aidha, Wizarainatoa shukranizadhati kwa wote walioshiriki kuandaa kitini hiki na inawaomba washiriki pia kuwezesha mijadala inayoandaliwa katika ngazi ya jamii.



Dkt. Seif. A. Shekalaghe

**KATIBUMKUU**

# SURAYAKWANZA UTANGULIZI

## Usuli

Kitini hiki kimeandaliwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wawezeshaji wa majadiliano ya mila na desturi yatakayofanyika katika ngazi ya Jamii ili kubaini na kuibua mila na desturi chanya zinazosaidia kutokomeza vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto zinazopaswa kuendelezwa na mila na desturi hasi zinazochochea vitendo vyaukatili kwa wanawake na watoto ili zitokomezwe. Baadhi ya madhara ya mila na desturi ni vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake vikiwemo ukeketaji, ndoa zautotoni,utakasajiwawanawakenawatotowakike pamoja na kutoruhusiwa kurithi mali katika jamii.

Kitini kitasaidia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji wa majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii wa Mwaka 2022, ambaouliandaliwakwaajiliyakutekelezasehemuya pili ya Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto wa Mwaka 2016/17 hadi 2021/22. Mpango huo umefanyiwa mapitio ambapo umeandaliwa Mpango wa Pili unaotekelezwakuanzia mwaka 2023/24 hadi 2027/28.

Kitini kitawezesha wadau mbalimbali kuwa nauelewa wa pamoja wa namna ya kuendesha majadilianoyatakayowezeshajamiikuibuamilana

desturichanyazinazopaswakuendelezwanamila na desturi zenye madhara zinazopaswa kutokomezwa. Aidha, wakati wa majadiliano jamii inatarajiwa kuandaa mpango kazi wenye afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

## MalengoyaKitini

Malengoyakitinichawawezeshajiwamilanadesturi ni:

i. Kuwajengea uwezo wawezeshaji wa kuendesha majadilianoyaMilanaDesturingaziyaJamii;na
ii. Kutoa mwongozo wa kuwezesha majadiliano ya mila na desturi ngazi ya jamii ili kuibua Mila na Desturi chanya zinazopaswa kuendelezwa na mila na desturi hasi zinapaswa kuachwa ili kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto.

## Matumiziya Kitini

Kitini hiki kitatumiwa na wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa jamii, Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Dini, Makundi ya Kujitolea ya Uwezeshaji wa Mila na Desturi, Wanajamii wawezeshaji na wadau wengine wanaowezesha mijadala ya Mila na Desturi.

## WawezeshajiwaMajadiliano

Mwezeshaji ni mtu muhimu katika kufanikisha majadiliano kuhusu athari chanya na hasi za Mila na Desturi katika Jamii. Kwa kuzingatia unyeti wa majadiliano ya Mila na Desturi, yeyote kati ya makundi yaliyotajwa katika 1.3 ni lazima awe:

i. Anafurahiakufanyakazindaniyajamii;
ii. Ana taarifa sahihi za mila, desturi na mienendo ya jamii atakayoihudumia;
iii. Nautayari wakuwamwezeshaji;
iv. Na stadi nzuri za mawasiliano na kuwezesha kikundi ndani ya jamii;
v. Msikilizaji mzuri mwenye uwezo wa kupokea na kuvumilia maoni tofauti;
vi. Naamanianapojadilimasualayamilana desturi za jamii;
vii. Nauwezowaucheshiwakiasi;
viii. Na uwezo wa kutumia mbinu shirikishi wakati wa kuongoza majadiliano katika jamii;
ix. Na uwezo wa kuboresha mafunzo, vitendo na mazoezi kulingana na mazingira ya jamii husika; na
x. Na uwezo wa kuhamasisha majadiliano ili wanajamii waweze kutambua mila na desturi chanya na hasi katika jamii husika.

## SURAYAPILI: MWONGOZO WATAIFAWA UENDESHAJI MAJADILIANO KUHUSIANA NA MILANADESTURIZENYEMADHARAKWAJAMII WA MWAKA 2022

Sura ya pili ya kitini inalenga kuwapitisha wawezeshaji wa majadiliano ya Mila na Desturi kwenye Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji wa Majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii wa Mwaka 2022, ili kujua maudhui ya mwongozo ikiwemo namna ya kuendesha majadiliano, mbinu zitakazotumika na matokeo.

| | **Maelezoya Mjadala** | **Muda: Dakika90** |
|---|---|---|
| **Utangulizi** | Mwongozo huu ni sehemu ya utekelezajiwaeneolapiliyaMpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili DhidiyaWanawakenaWatotowa mwaka2016/17hadi2021/22. | |
| **Malengo** | Kufikia mwishowamajadiliano haya washiriki wanatarajiwa kuweza:-<br>i. Kutumia mwongozo kwenye mijadala ndani ya jamii,<br>ii. Kuelezadhananzimailiyopokatika mwongozo huu, na<br>iii. Kujadili majukumu ambayo wanatarajiwakufanyakatikajamii | |

| | |
|---|---|
| **Mbinu za Uwezeshaji** | Tumia mbinu za uwezeshaji ambazo ni shirikishi. Kumbuka kuwa washiriki wana ufahamu fulani kuhusu mwongozo huu. Kwa hiyo mbinu zitakazotumika katika somo hili ni pamoja na:-<br>i. Majadilianokwavikundi;<br>ii. Kuwasilisha matokeo ya majadiliano kwa kundi kubwa;<br>iii. Majadiliano ya wote katika kundi kubwa;<br>iv. Kutumia mhadhara shirikishi kutoa taarifa sahihi na kuhitimisha; na<br>v. Hitimishakwakutoataarifa sahihi |
| **Zana/vifaa vya kufundishia** | Daftari, kalamu, kalamu za bangokitita, karatasi zenye kunata, bangokitita, stendi ya bangokitita, kalamuzakuchorea,projektana kompyutampakato. |

| | |
|---|---|
| **Shughuliza Mwezeshaji nawashiriki** | i. Wagawe washiriki katika makundi manne wafanyewajadili kama ifuatavyo:-<br>(a) Kundilakwanza: Madhumuniyamwongozo<br>(b) Kundi la pili: Waeleze matumizi ya mwongozo huu<br>(c) Kundi la tatu na la nne: wajadili mambo ambayo mwongozo unalenga kuyasahihisha katika jamii<br>ii Baadayamajadilianoyadakika 10 waombe kila kundi kutoa mrejesho wa kundi lao,<br>iii Ongoza majadiliano ya kuchambuamwongozo,na<br>. Hitimishakwakutoataarifasahihi. |

| | |
|---|---|
| **Mpangilio wa uwezeshaji** | Mtiririkowakuwezeshamajadiliano utakuwa kama ifuatavyo:<br><br>i. ElezamalengoyaMjadala<br>ii. Kisha tumia mhadhara shirikishi ili:<br><br>(a) Kueleza chanzo cha mwongozo kwa kuoanisha na Mpangowa Taifa wa kutokomeza ukatilidhidiya wanawake na watoto wa 2016/17 hadi 2021/22,<br>(b) Kueleza madhumuni ya kuandaa mwongozo huu,<br>(c) Kueleza maudhui ya kila mada kwa kifupi, na<br>(d) Kueleza mambo ambayo mwongozo unalenga kuyatokomesha<br><br>iii. Tathmini uelewa mwongozo kwa kutumia mfumo wa maswali na majibu,<br>iv. Hamasisha washiriki kuuliza maswali, na<br>v. Hitimishamjadalakwakutoa taarifazanyongeza |

| | |
|---|---|
| **Ushauri kwa mwezeshaji** | Mwezeshaji hana budi kuheshimu tofauti za kiimani, kidini, kimila na desturi za washiriki na kuwawezesha washiriki kujua kwamba wana haki kuhusiana na maadili, imani na maoniyaonasilazimakilamtu kushirikikatikaimaniyamwingine. |

**RejeayaMwezeshaji**

**UmuhimuwaMwongozo**

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ili kushughulikia, pamoja na mambo mengine, Mila na Desturi zenye kuleta madhara kwa jamii.Mpango huu ulijikita katika maeneo ya utekelezaji manane (8) ambapo mojawapo ya afua zilizo katika Mpango huo ni kuandaa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara katika Jamii.

Mwongozo huu umeandaliwa ukiwa na taarifa, maarifa, mbinu, lugha rahisi na maelezo ya hatua za kufuata ili kufikia Malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Mwongozo huu ni matokeo ya mashauriano ya kina yaliyofanywa na Serikali, Wananchi pamoja na WadauwaMaendeleokatikaeneolaMilanaDesturi.

## Madhumuniya Mwongozo

MwongozounalengakukuzanakuimarishaMilana Desturi chanya zinazowezesha jamii kujenga mahusiano mazuri yenye kuleta heshima na yanayozingatia usawa wa kijinsia, hivyo: -

i. Kuiwezesha jamii kutambua na kuendeleza mila na desturi chanya zinazoimarisha usawa wa kijinsia;
ii. Kusaidia jamii kutambua na kukabiliana na mila na desturi zinazoendeleza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
iii. Kuiwezesha jamii kufikia muafaka na kuweka mikakati ya pamoja ya kutokomeza mila na desturi zenye madhara katika jamii;
iv. Kukuza na kuiwezesha jamii kuibua na kutekeleza mbinu shirikishi za kutokomeza vitendo vya ukatili; na
v. Kuandaa jukwaa kwa ajili ya kuwezesha makundi maalum hususan wanawake na watoto kupaza sauti zao.

## Matumiziya Mwongozo

Mwongozo utatumika kama nyenzo ya kusaidia jamii kufanya majadiliano ya pamoja kuhusiana na Mila na Desturi chanya zinazotakiwa kuendelezwa na zile zenye kuleta madhara katika jamii zinazopaswa kutokomezwa ili kupunguza pengo la usawa wa kijinsia.Mwongozo unalenga kuongeza chachu ya utekelezajiwaMpangoKaziwaTaifawa

Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Walengwa wa Mwongozo huu ni pamoja na Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Viongozi wa kimila, Viongozi wa dini, Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Kidini na Kijamii ambayo hupanga na kuendesha majadiliano ngazi ya jamii ili kuimarisha uwezo wa jamii katika kuendeleza Mila na Desturi nzuri na kukabiliana na zile ambazo zinachochea na kuendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

**MilanaDesturiAmbazoMwongozo Unalenga Kuzitokomeza/Kukabiliana**

Kuna Mila na Desturi ambazo bado ni changamoto kwa makuzi ya watoto na vijana balehe, ikiwemo kulazimishwa kwa watoto kuoa au kuolewa mapema naukeketajikwa wasichana. Milana Desturihizizina madhara katika afya ya uzazi kwa kundi hilo. Pia, wasichana wanaopata mimba katika umri mdogo wanakuwa hawajakomaa vizuri kiakili na kimaumbile kuwezakumudumajukumuyauzazinahivyo,kupata matatizo ya uzazi na kushindwa kumudu maisha.

Ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni pia zina athari kubwa katika afya, elimu na maendeleo ya wanawakenamtotowakikenahivyokuzorotesha

ushiriki wao katika maendeleo ya familia na nchi kwa ujumla.

**Mpangiliowa Mwongozo**

Mwongozo wa Taifa wa uendeshaji Majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi zenye madhara kwa Jamii uko katika mpangilio ufuatao:

i. **Sura ya kwanza** inaelezea utangulizi kuhusu mwongozo huu, malengo mahsusi, majukumuna wajibu wa wadau mbalimbali;
ii. **Sura ya pili** inatoa maelezo ya kina kuhusu mchakato mzima wa uendeshaji Majadiliano ya Kijamii;
iii. **Sura ya tatu** inahusu Mwongozo kwa wawezeshaji ambapo mbinu na kanuni mbalimbali za uwezeshaji zimefafanuliwa;
iv. **Sura ya nne** inatoa maelezo kuhusu kupangana kuendesha Majadiliano yenye ufanisi Ngazi ya Jamii; na
v. **Sura ya tano** inaangazia utunzaji wa kumbukumbu, ufuatiliaji na tathmini.

Mwishoni mwa Mwongozo huu kuna viambatisho vyenye mada mbalimbali muhimu za kufundishia.

**Ujumbe Muhimu**: Zingatia Mwongozo wa Taifa wa Kuendesha Mjadiliano Kuhusu Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii.

## SURA YA TATU

## USHIRIKISHWAJIWAJAMII

Sura ya tatu ya kitini inalenga kuwakumbusha wawezeshaji wa Mila na Desturi umuhimu wa kushirikisha jamii kwa njia ya mjadala ili kutafuta suluhisho la changamoto ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaochangiwa na Mila na Desturi hasi. Kwa upande mwingine kuzitambua zile nzuri zinazosaidia kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili ziendelezwe. Aidha, katika hatua hii wawezeshaji watatambulishwa dhana ya kuendesha majadiliano kwenye jamii (Community Dialogue)kamanyezomuhimuyakujengauwezowa jamii kujiamini na kushiriki kutoa mawazo, maoni na mapendekezo ya kutatua athari za ukatili zinazobabishwa na mila na desturi.

| | **MaelezoyaMada** | **Muda: Dakika90** |
|---|---|---|
| **Utangulizi** | Wawezeshaji watajua namna ya kufuata taratibu za kuingia kwenye jamii bila kupata vikwazo ikiwemo kuwasiliana na viongozi wa eneo husika ili kupata kibali cha kuweza kuendesha majadiliano. Vilevile, majadiliano yatawasaidia wawezeshaji kufahamu umuhimu wa kutodharau au kutumia lugha za majingambo wanapokuwa wanafanya kazi kwenye jamii, watajua umuhimu wa kujishusha ili ujumbe uweze kufika kwa jamii na kutendewakazikwaajiliya mabadilikoyaliyokusudiwa. | |
| **Malengo** | Kufikia mwisho wa majadiliano washiriki wataweza:-<br>i. Kueleza umuhimu kushirikisha jamii.<br>ii. Kutumiambinushirikishikatika uwezeshaji.<br>iii. Kuendesha majadiliano ngazi ya jamii.<br>iv. Kuandaa mahali pa kufanyia majadiliano. | |

| | |
|---|---|
| **Mbinu za Uwezeshaji** | Tumia mbinu za uwezeshaji ambazo ni shirikishi. Kumbuka kuwa washiriki wana ufahamu fulani kuhusu mwongozo huu. Kwa hiyo mbinu zitakazotumika katika kuwezesha majadiliano ni pamoja na:<br>vi. Majadilianokwavikundi;<br>vii. Kuwasilisha matokeo ya majadiliano kwa kundi kubwa;<br>viii. Majadiliano ya wote katika kundi kubwa;<br>ix. Kutumia mhadhara shirikishi kutoa taarifa sahihi na kuhitimisha; na<br>x. Hitimisha kwa kutoa taarifa sahihi. |
| **Zana na vifaa vya kufundishia** | Daftari, kalamu, *makerpen*, karatasi zenye kunata, bangokitita, stendi ya bangokitita,kalamuzakuchorea, projektanakompyutampakato. |

| | |
|---|---|
| **Shughuliza Mwezeshaji na washiriki** | i. Wagawe washiriki katika makundi matatu wafanyewajadili kama ifuatavyo:-<br>(a) Kundi la Kwanza:Wajadili maana ya ushirikishwaji jamii;<br>(b) Kundi la pili: Umuhimuwa kushirikisha jamii;<br>(c) Kundi la tatu: Wajadili athari za kutoshirikisha jamii; na<br>(d) Umuhimu wa kuendesha mijadala katika jamii.<br>ii. Baadayamajadilianoyadakika 10 waombe kila kundi kutoa mrejesho wa kundi lao;<br>iii. Ongoza majadiliano ya kuchambua kazi zilizowasilishwa;na<br>iv. Hitimisha kwa kutoa taarifa sahihi. |

| | |
|---|---|
| **Mpangilio wa uwezeshaji** | Katika kuwezesha mjadala mtiririko utakuwa kama ifuatavyo:-<br>i. Ongoza zoezi la kazi ya vikundi na kupata matokeo yake;<br>ii. Kisha tumia mhadhara shirikishi ili;<br>(a) Kueleza maana ya ushirikishwaji jamii;<br>(b) Kueleza umuhimu wa kushirikisha jamii;<br>(c) Kueleza athari za kutokushirikisha jamii; na<br>(d) Kueleza umuhimu wa kuendesha mijadala kwenye jamii.<br>iv. Tathmini uelewa wa mada kwa kutumia mfumo wa maswali na majibu;<br>v. Hamasisha washiriki kuuliza maswali; na<br>vi. Hitimisha mada kwa kutoataarifa za nyongeza. |
| **Ushauri kwa mwezeshaji** | Mwezeshaji azingatie maelekezo, kanuni, na taratibu za uwezeshaji. |

**TaarifazaMwezeshaji**

**Ushirikishwajijamii**

Ushirikishwaji wa jamii ni mchakato wa jamii kushiriki kwenye hatua zote za kutatua changamoto au kuanzishamiradiauprogramuzamaendeleo

kuanzia wazo, upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini.

Hatua hii hufikiwa pale jamii inapotambua uwezowao katika kutafuta majawabu ya changamoto ikiwemo mila na desturi zinazochochea vitendo vya ukatili wa wanawake na watoto. Jamii inakuwa na uwezo wa kufahamu walipo na kuamua wanapotaka kwenda na kuandaa mpango wa utekelezaji kwa njia ya kujitegemea.

**FaidazaKushirikisha Jamii**

Faidazakushirikishajamiinihizizifuatazo:-

i. Kuwanauelewawapamoja;
ii. Kufanya maamuzi bora – kushirikisha jamii huleta taarifa na mitazamo inayosaidia kufanya maamuzi makubwa na matokeo kwa wadau wote;
iii. Uwajibikaji wa pamoja katika jamii – kushirikisha jamiikunajengauwajibikawapamojanakufanya kazi kwa timu;
iv. Kujenga kuaminika – kuwasiliana ipasavyo na wanajamii hujenga uwazi na kusaidia kujenga kuaminika;
v. Kukubalika kufanya kazi ndani ya jamii – huongezeka kuaminika na huleta matokeo chanya; na
vi. Utatuzi wa migogoro – kushirikisha jamii huwezeshakuainishasehemuzenyemigogoro

mapema, na kukubaliana namna ya kutatua migogoro hiyo.

**AtharizaKutoshirikishaJamii**

Waeleze washiriki athari ambazo zaweza kutokea kama taratibu za kushirikisha jamii hazitazingatiwa; athari hizo ni pamoja na kutokukubalika kwenye jamii husika, kukosa ushirikiano na hivyo kushindwa kufikisha ujumbe uliokusudiwa.

**MjadalaKatikaJamii**

Mjadala katika jamii ni dhana inayojenga uwezo wa jamii kujiamini, kuelewa ukweli na kufunguka kuhusu ukweli wa changamoto zinazowakabili katika maisha ikiwemo athari ya Mila na Desturi zinavyochangia ukatili wa wanawake na watoto.

**Lengo:**Mijadalakatikajamiinijukwaakwa wanajami hususan wazazi, walezi, vijana balele, viongozi wa jamii, viongozi wa kidini na kimila kujadili na kupendekeza namna ya kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto.

**UmuhimuwaMijadalakatikaJamii**

(i) Mjadala katika jamii ni mchakato jumuishi wa utambuzi na uchambuzi wa changamoto katika jamii ili kuboresha na kutoa mwelekeo mpya wa kukabiliana na changamoto;

(ii) Mjadala katika jamii ni mchakato jumuishi na shirikishi wa kupeana taarifa kati ya watu au

vikundi ili kuwa na uelewa wa pamoja na ufumbuzi stahiki wa changamoto;

(iii) Mijadala husaidia kujenga uwezo wa jamii kutambua Mila na Desturi hasi, kuwa na uelewa wa ndani kuhusu visababisho na kuchukua hatua ya mageuzi ya fikra na mtazamo; na

(iv) Dhana hii inawezesha uwajibikaji badala ya kumnyoshea kidole mtu mwingine na kuwa na makubaliano ya pamoja ya kutatua changamoto. Mijadala inajenga umoja katika kutatuta suluhisho ya changamoto.

# SURAYANNE

# KUENDESHAMAJADILIANOYAMILANA DESTURI NGAZI YA JAMII

Sura ya nne ya kitini inalenga kuelezea maandaliziya majadiliano kwenye jamii, zana na mbinu zitakazotumika kuendesha majadiliano, namna ya kuendesha majadiliano pamoja na mpango kazi wa kushughulikiachangamotozaukatilizitakazojitokeza.

## Kupangamajadilianongaziyajamii

### Taratibu za Kuzingatia Kabla ya Majadiliano

Taratibu zote muhimu zinazohitajika kabla yakufanya majadiliano zinapaswa kuzingatiwa na mwezeshaji wakati wa kuandaa majadiliano ngazi ya jamii. Hii ni pamoja na kupata ruhusa kutoka kwa mamlaka husika. Uongozi wa eneo linalokusudiwa la kijiografia unapaswa kufahamishwa kupitia mawasiliano rasmi.

### (i) Walengwa

Kitini kinalenga kuleta mabadiliko chanya kwa watu wenye ushawishi katika jamii, waendelezaji wa vitendovyaukatili,waathirikawaukatilinawalewalio katika hatari ya kufanyiwa ukatili hususan wanawake na watoto.

Uchaguzi wa washiriki kwa ajili ya majadiliano ngazi ya jamii unapaswa kuzingatia vikundi tofauti vya kijamii. Miundo ya kijamii inayopewa kipaumbele ni ile inayochukuliwa kuwa walezi na waendelezaji wa Mila na Desturi katika jamii kama vile Viongozi wa Kidini, wazee/viongozi wa jamii, wanaume na wavulana, pamoja na vikundi vya wanawake na wenye ulemavu..

Viongozi wa jamii, watashirikiana na mwezeshaji kuteua wanajamii watakaoshiriki katika majadiliano. Ikiwawanajamiiwotewanatakakushiriki,mwezeshaji atamshauri kiongozi wa jamii kuja na vigezo vya uteuzi wa washiriki wa kikao cha majadiliano.

### (ii) Mialiko

Mialiko inapaswa kuwa wazi na kutolewa kwa wakati (zaidi ya wiki moja kabla) ili kuepuka mkanganyiko. Mialiko inaweza kuwa kupitia barua au ujumbe wa mdomo kutoka kwa mtaalam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa aumashirika ambayo yanawezesha majadiliano ili kuthibitisha uhalali.

### (iii) MahalipaKufanyiaMajadiliano

Majadilianongazi yajamiiyanawezakufanyikakatika maeneo mbalimbali. Wakati wa kuchagua mahali pa kufanyia majadiliano, ni muhimu kwa mwezeshaji kuzingatia yafuatayo:-

a) Usalama wa eneo na nafasi kwa ajili ya usirina faragha ya washiriki;
b) Viti vinavyoweza kupangwa kwenye duara ili kutoa hali ya usawa miongoni mwa washiriki, kuruhusu washiriki kutazamana ana kwa ana na kuhimiza majadiliano ya wazi; angalia Mila na Desturi zinaoongoza ukaaji wa wanaumena wanawake kwenye jamii husika; na
c) Muda unaopangwa kwa ajili ya kuwezesha majadilianongaziyajamiiuzingatiekalendaya msimu.

**Kuwezesha majadiliano kwenye jamii** Sehemu zilizotangulia za kitini zimelenga kumwezeshamwezeshajikuwanaujuzinauwezo wa kuwezesha majadiliano ya Mila na Desturi katika ngaziyajamii,katikahatuahiiyakitinimwezeshaji anakuwa tayari kuwezesha majadiliano kwa kutumia mbinu shirikishi zinazotoa fursa kwa wanajamii/kikundi kushiriki moja kwa moja kwenye majadiliano na kutoa maoni na suluhisho la changamoto zinazojadiliwa. Ieleweke kuwa uchaguzi wa mbinu zitakazotumika kuwezesha majadiliano zinategemeana na mazingira ya eneo yatakapofanyika majadiliano ikiwemo shughuli za kijamii na kiuchumi, Mila na Desturi na hatua ya maendeleo iliyofikiwa.

Mbinu/zana za kuwezesha majadiliano ni kama zifuatazo:-

### (i) Zana: Historia ya Matukio Muhimu ya Kijiji/Mtaa

Zana hii huwezesha washiriki kuelezea matukio muhimukwenyekijiji/mtaaambayoyanagusamaisha ya watu yakiwemo ya Mila na Desturi.

**Lengo**:-Kujifunzamatukioyakihitoriayenyefaidana madhara kwa maisha ya jamii na namna kuwezesha jamii kutafuta kinga au ufumbuzi ikiwepo ukatili wa wanawake na watoto.

**Hatua:-**

(a) Mwezeshaji aanzishe mazungumzo kwenye kikundi mahsusi kwa kuwauliza matukio muhimu wanayokumbuka kutokea ndani ya kijiji/mtaa (mazuri na mabaya);

(b) Wawezeshe wayataje kwa kufuata miongo au miaka kadri wanavyokumbuka;

(c) Watajefaidanahasarazamatukio;

(d) Waelezewalichukuahatuaganikutatuaaukukab iliana nayo;

(e) Kamatukiozuriwaombewaelezemafanikio yaliyopatikana; na

(f) Andaa jedwali la matukio ya kihitoria ya kijiji/mtaa.

**Jedwali Na. 1:** Historia ya matukio ya Mila naDesturi katika kijii/Mtaa xxxxxxxx

| Mwaka | Tukio | Sababisho | Madhara/ Manufaa | Ufumbuzi/ Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

### (ii) Zana: Uchambuzi wa Mahusiano Kati ya Taasisi na Taasisi na Makundi Mbalimbali (VENN Diagram)

Uchambuzi wa Kitaasisi ni zana inatumika kuelewa mahusiano ya taasisi au makundi mbalimbali yaliyopo katika jamii. Zana hii huwezesha washiriki kujadili na kutambua makundi yenye nguvu na maamuzi kuhusu jamii. Majadiliano ya Mila na Desturi yatasaidia kuelewa watu wenye mamlaka, maamuzi na umiliki wa Mila na Desturi za eneo na kuwafanya kuwa sehemu ya kutafuta suluhisho la Mila na Desturi hasi zinazochochea ukatili wa wanawake na watoto.

**Lengo**: Kuwezesha washiriki kutambua na kuchambua mahusiano baina ya taasisi na makundi mbalimbali kwenye jamii na namna yanavyochangia kuwepo kwa Mila na Desturi zuri zinazopaswa kuendelezwa na hasi zinazopaswa kuachwa ili kutokomeza vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto.

**Hatua:-**

a) Tambulisha zoezi la kujadili na kuchambua mahusianoyakitaasisi,makundimbalimbalina jamii kuhusu Mila na Desturi katika jamii husika. Fafanua kuwa zoezi hili ni muhimu katika kutambua watu au makundi au taasisi zenye mamlaka, maamuzi na umiliki wa mila na desturi kwenye Jamii;


b) Wagawe washiriki katika makundi matatu, kila kundi liorodheshe Taasisi, makundi au watu wenye mamlaka, maamuzi, umiliki na ushawishi kuhusu Mila na Desturi. Pia wataje hata ambao hawana maamuzi, wala mamlaka, umiliki na ushawishi wa Mila na Desturi za eneo;

> Mfano:WazeewaMila,wazeewaukoo, waganga wa jadi, mangariba, serikali za kijiji, Kanisa, Msikiti, Shule ya sekondari, Shule ya Msingi, sungusungu, viongozi wa koo, Kamati ya Mpango wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, Baraza la watoto, Vikundi vya Malezi, wazazi, Shirika lisilo la kiserikali na Halmashauri ya Wilaya.
>
> NB: Usiwalazimishe kutaja bali wafanye wakumbukemakundiyoteyandaninanjeya kijiji.

c) Washiriki wajadili na kukubaliana juu ya umuhimu wa taasisi au kikundi na mchango wake katika Mila na Desturi;

d) Wawezeshe washiriki kukata kadi za ukubwa mbalimbali zikiwemo kubwa, za kati na ndogo na waandike taasisi au kundi au mtu katika kadi kulingana na umuhimu, mamlaka, maamuzi na ushawishi kwenye Mila naDesturi;
e) Washiriki wachore mduara mkubwa ardhini na waanze kupanga kadi kuanzia kwenye kitovu cha mduara kwa umuhimu, mamlaka, maamuzi, umiliki na ushawishi wa Mila na Desturi kwenye jamii na vigezo vingine watakavyovitaja;
f) Waelekeze washiriki kupanga kadi katika mduara (chapati) umbali wa kadi toka katika kitovu cha mduara ni kiashirio cha kutokuwana maamuzi na nguvu katika maamuzi na matukio ya Kimila na Desturi katika jamii husika; na
g) Wawezeshe washiriki wajadili na kutoa maelezo ni kwa nini wamezipanga kadi katika nafasi hizo (Mchoro).

MfanowaMchoroNa.1:-Mahusianobainayajamii katikamasualayaMilanaDesturi na Taasisi au kikundi



h) Baada ya kukamilisha mchoro na uchambuzi washiriki wapange matokeo ya uchambuzi kwenye jedwali hapo chini.

Wawezeshe jamii kupanga matokeo ya uchambuzi katika jedwali.

Jedwali Na.2: Uchambuzi wa Mahusiano kati ya Taasisi, Makundi mbalimbali na Jamii katika Kijiji/Mtaaxxxxxx

| **Taasisi/Kikundi/Mtu** | **Shughuli** | **Umuhimu** | **Mapungufu** |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

NB:- Mwisho wa majadiliano washiriki watatambua makundi yenye ushawishi kuhusu Mila na Desturi na kuona namna ya kuyatumia kubadili fikra na mtazamo kwenye jamii kuhusu Mila na Desturi.

### (iii) Zana:Majadiliano yaKundiLengwa

Majadiliano ya kundi lengwa yanahusisha watu wenye wasifu na uzoefu unaofanana kujadili mada muhimu (ikiwepo umri, uwezo wa kipato, uelewa na uzoefu juu ya jambo linalojadiliwa n.k).

Majadiliano huongozwa na mwezeshaji ambaye hutambulisha mada na kuwezesha wanakikundi kushiriki vyema kwa uhuru katika mjadala.

Ili kuhakikisha kwamba kila mtu anasikilizwa wakati wa majadiliano, idadi ya washiriki haipaswi kuzidi watu 25-30 kutegemeana na mpangilio wa majadiliano. Idadi ya watu ikizidi 30, itamwia vigumu mwezeshaji kuhakikisha ushiriki wa kila mtu katika majadiliano.

Zana hii huwezesha washiriki kukubaliana au kutokubaliana na inatoa fursa ya kuonesha namna wanakikundi wanavyotazama jambo linalojadiliwa, maoni na mawazo tofauti, na tofauti zilizopo kuhusu Mila na Desturi, uzoefu na kinachofanyika kwenye jamii husika.

**Hatua:-**

a) Waalike wanakikundi wenye wasifu na uzoefu unaofanana, zingatia na umri;
b) Tambua lengo la majadiliano ya kundi lengwa, andaa maswali ya msingi, andaa ajenda na panga namna na kuandika mhutasari wa majadiliano;

**Mfanowa mada:**

*“Mila na desturi nzuri zinazosaidia kutokomeza ukatili zinazopaswa kuendelezwa”*

*“Milanadesturizinazochangiaukatiliwawanawake na watoto zinazopaswa kutokomezwa”*

**Dondoo zakuongozaMajadiliano**

Kwakawaidamajadilianoyakundilengwahuwa

hayaongozwi na mwenyekiti bali mwezeshaji ambaye huandaa dondoo za maeneo ya majadiliano. Pia miongoni mwa wawezeshaji anaandika yanayojitokeza kwenye mjadala.

**Mfanowa dondoo**

JemnafahamuninikuhusuMilanaDesturikatika kijiji au mtaa wenu?

Ni Mila na Desturi zipi zilizopo kwenye kijiji chenu au mtaa wenu? Ikiwezekana kila mshiriki ataje Mila na Desturi anazozifahamu.

Katika mila zilizopo ni zipi ambazo zinasaidia kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto? Waeleze na sababu kwa nini zinasaidia.

Ni mila zipi ambazo zinachochea ukatili wa wanawake na watoto katika kijiji chenu au mtaa wenu? Waeleze na sababu.

Ni Taasisi ipi au kundi lipi? Mtu mwenye mamlaka, maamuzi na umiliki wa Mila na Desturi kwenye kijiji chenu au mtaa wenu? Waeleze sababu

Ni athari zipi zinazopatikana kupitia Mila na Desturi kwa wanawake na watoto? Waeleze na sababu.

Mwezeshaji andaa kwa uangalifu maneno au lugha itakayotumika katika kuuliza maswali, usiwe na upande wakati wa majadiliano na mwisho toa mhutasari wa yaliyojitokeza katika majadiliano.

c) Baada ya mjadala wa kina waandae jedwali la mpango kazi wa nanma ya kutatua changamoto za Mila na Desturi na namna ya kuendeleza zile ambazo ni nzuri.

| Mila/Desturi | Sababisho | Madhara/ Manufaa | Ufumbuzi/ matokeo |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

### (iv) Zana:Igizodhima

Igizo dhima ni mbinu ambayo kwa Mwezeshaji huwapa washiriki hali ambazo washiriki hufanyia igizo. Mwezeshaji anachagua hali ambayo inafahamika kwa washiriki ili waweze kuigiza. Wakati anawapa hali hiyo ya kuigiza ahakikishe kuwa malengo ya igizo yanaeleweka kwa wote. Inashauriwa kuwa washiriki wajitolee kuigiza – mwezeshaji asiwachague. Baada ya igizo washiriki wote watoe mrejesho wa walichojifunza. Mwezeshaji aongoze majadiliano kwa kutumia maswali aliyoyaandaa awali.

Pia hutumika kuelewa zaidi mitazamo/tabia za wengine ili kuanzisha mabadiliko ya mitazamo/tabia. Mwisho hutumika kutathmini utendaji kwenye hali fulani kwa nia ya kuboresha.

Matumizi ya igizo dhima yanamtaka Mwezeshaji kuwa mwangalifu sana kama ifuatavyo:-

a) Kwanza ni lazima ahakikishe kuwa Igizo dhima linahusu malengo ya mada, lina uhalisia wa kupambanua tatizo, linahamasisha na linatoa changamoto kwa wachezaji na watazamaji.

b) Pili, kabla ya kuanza Mwezeshaji hana budi kueleza hali ya kisa ilivyo, kuleza wajibu wa kila mchezaji, kuandaa mwongozo wa masuala ya kuangalia kwa watazamaji na kuandaa mpango wa kuendesha majadiliano ili kuibua mafunzo muhimu.

c) Baada ya kukamilisha taratibu za igizo dhima Mwezeshaji aongoze walioshiriki kwenye igizo dhima kujivua nafasi walizocheza kwa kusema “Mimi siyo … tena bali ni …” (Hii ni muhimu kwani igizo dhima linaweza kuleta hisia kali ambazo mshiriki anaweza kukaa nazo kwamuda mrefu).

Zanaaumbinuhiiitumiketupaleambakokatika jamii yanapowezesha majadiliano ina watu wenye uwezo wa kufanya igizo dhima la Mila na Desturi na kuleta mazingira ambayo yataibua mjadala. NamarabaadayaigizodhimaMwezeshajiaendeshe majadiliano kwa kuwauliza washiriki maswali yafuatayo:-

Jemmejifunzaninikuhusuigizo?

Nisehemuipizaigizodhimamlifurahia?Nakwa sababugani?

Ni sehemu zipi za igizo dhima ambazo hamkufurahia?Nakwasababugani?

Nini kifanyike kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwenye igizo dhima?

### (v) Zana: Kisa

Kisa kilivyo ni kama hadithi. Kinaanza na kuelezea hali iliyopo na kisha huonyesha matukio kadhaa yaliyojitokeza katika hali hiyo. Tofauti na hadithi ya kawaida, kisa huwa hakina mwisho maalum. Watu wanaombwa kutoa maamuzi au kujadili jinsi ya kuziba mapengo yaliyojitokeza. Mfano watu wanaweza kuuulizwa hatua ambazo wahusika

katika kisa wangeweza kuchukua baadaye, wangekuwa na hisia zipi?, mwenendo waoungekuwa upi? Nk.Watu pia wangetakiwa kutoa maoni yao juu ya mwenendo wa wahusika katikakisa na kupendekeza ushauri kwa wahusika.

### WakatiwaKutumiaKisa

Madhumuni ya Kisa ni kuwafanya watu wafikiri na kujadili njia nzuri zaidi za kutatua matatizo. Kwa kufanyahivikisakinawezakuwasaidiawatu

kuyagunduanakuyaelewavizurizaidimatatizona sababu zake?

KISA No.1

Katika kijiji cha Songambele, wapo wazee wengi ambao ni maarufu sana kutokana na sifa mbalimbali walizojijengea kwa miaka mingi. Sifahizi ni kama vile idadi kubwa ya mifugo, ukulima hodari na utajiri. Kwa upande wa kijiji chetu unapozungumzia Mzee Tumaini hutashangazwa kufahamu kuwa ni mtu wa aina yake. Anafahamika na vijana na wazee wengi katika kijiji chetu. Yeye anazo sifa nyingi kama vile sifa ya ulengajishabaha kwa kutumia mkuki na manati. Vilevile ni mtu jeuri sana, mnene na mweusi. Unaweza kumfananisha na askari waliopigana vita vya majimaji. Mzee Tumaini anao watoto wengi wa kiume na kike.

Yeye hupenda sana watoto wa kiume kuliko wa kike, kwa sababu zake binafsi. Vilevile miongomi mwa watoto wa kike, mmojawapo ni mlemavu na amesahaulika katika kupewa elimu na matunzo. Yeye anaamini ya kuwa watoto wa kike siku zote ni hasara. Watoto wote wa kiume amewasomesha katika sehemu mbalimbali nchini na nje ya nchi na watoto wakikehanahabarinao,jukumulakuwalea amewaachia wake zake.

Kwa uhakika hajawasomesha hata kidogo. Yeye anachokitilia maanani kwa binti zake ni kuwafanyia tohara (kuwakeketa) ambayo anaamini huwaondoleamikosi.Yeyenimiongonimwa

wazaziwanaoozeshawatotowakikekatikaumri mdogoiliapate mahari.

Sikuzahivikaribunialiitwanakamatiyashule ikimhimiza awaandikishe shule binti zake. Inavyoonekana ameziba masikio kabisa. Kwa sababuhiyokamatiyashuleiliamuakumfikisha katika vyombo vya sheria. Lakini pamoja na kufikishwa katikavyombovya SheriaMzeeTumaini ni mjeuri kama chui na ameamua kutojihusisha na shughuli zozote za maendeleo kijijini kwa kisingizio kuwa anafutwa futwa na watu wasiomtakia mema katika maisha yake.

**Hatua**

a) Mwezeshajiahakikishekuwataarifailiyokwenye kisa hicho inatosheleza kwa washiriki kufanya majadiliano;
b) Mwezeshaji awape washiriki kisa na wakisome kwa makini. Kisha awaongoze washiriki kujadili kisa hicho na kutoa ufumbuzi ama kwa makundi au kwa pamoja. Mwisho anatoa hitimisho na maarifa mapya.

MfanowaMaswali

Jeumejifunzaninikatikakisa hiki?

Hali iliyopo katika kijiji cha Songambele, ipo katika kijiji au mtaa wenu?

Ninikifanyikeilikuzuiaaukutatuachangamotokama hizi?

c) Mwezeshaji atagawa washiriki katika vikundi vidogo vidogo na kila kikundi atakipa kisa; na

d) Wasome kisa, wajadilili na kuwasilisha kwenye majadiliano ya pamoja walichojifunza ikiwemo mambo mazuri, changamoto na mapendekezo ya kurekebisha hali iliyopo.

### (vi) MchezowaKuigiza

Mchezo wa kuigiza ni mbinu muhimu katika kuanzisha mjadala ngazi ya jami unaweza kuchezwa moja kwa moja au kurekodiwa sauti au video. Jamii ya sasa inapenda sana kuangalia tamthlia, kwa hiyo mchezo wa kuigiza kuhusu mila na desturi ukiandaliwa vizuri unaweza kuwa kivutio katika kuchokoza mjadala wa Mila na Desturi.

**MfanowaMchezowaKuigiza Washiriki**

1. Baba(BabaMamboleo)
2. Mama(Mama Mamboleo)

**MchezowaKuigiza**

Ni nyakati za saa saba mchana jua ni kali, baba na mama Mamboleo wapo shambani wakilima na wanaendelea kumalizia eneo lililobaki ili waanze safari ya kurudi nyumbani. Kwa mbali kidogo anasikikamatokeomwenyeumriwamiakamitatu

akiliakwasababuyajuakalinanjaa. Mwishoni mama Mamboleo anasikika akimwambia mumewe;

| | |
|---|---|
| **Mama Mamboleo:** | Baba Mamboleo! Samahani naona ni vema tuondoke sasa, maana naona mtoto analia kweli; ngoja nitangulie kurudi nyumbani nikaandae chakula. |
| **Baba Mamboleo:** | Mh! Ni kweli ngoja sasa tuondoke wote, kwa sababu naona huyu mswahili analia sana. Wee! Nyamaza watu unaona tumechoka halafu kelele hapa. Tutamalizia kesho. Hebu chukua na hili jembe tangulia nalo maana mimi nitapitia kwa Gendawuye nina shida kidogo! |
| **Mama Mamboleo:** | Sawamume wangu,Lakini…! |
| **Baba Mamboleo:** | Ngoja nikuongoze na hili shoka ulichukue lisije likapotea bure. Ukifika nyumbani tafadhali sana kabla ya kazi nyingine, chemsha maji ili nikifika tu niweze kuoga na niwahi kuondoka. Tumeelewana lakini? |
| **Mama Mamboleo:** | Sawa. Lakini mbona natakiwa niokote kuni, nichume mboga kwa ajili ya mlo wa jioni. Jamani baba matokeosisisotetumechoka.Hivi mwenzanguhuwezikuchukua |

|  |  |
|---|---|
|  | jembe, shoka na mtoto utangulie nayeilikaziiwe rahisi? |
| **Baba Mamboleo:** | Mama Mamboleo! Unataka kunieleza nini wewe? Ohoo!! Angalia usiniletee upuuzi wako hapa. Kwanza acha niondoke usije ukaniudhi bure. Mh! Wanawake bwana; nashindwa hata jinsi ya kuwaelekeza, Kila kitu! Desturi hii haipo kabisa katika familia na ukoo wetu. Elewa ni mwiko kabisa kumtuma mwanaume! |
| **Mama Mamboleo:** | Jamani!Yaaniunaonanikazindogo kubeba mtoto, majembe na shoka kwa wakati mmoja? Nitabebaje mizigo yote hii kwa wakati mmoja jamani? Hebu angalia. Mkononi nimebeba mboga, kichwani nimebeba kuni, mgongoni yupo mtoto, majembe na shoka nibebe wapi? Kwenye kiuno? Mh! hh! Ukisikia ule ukoloni wa kizamani, waliozungumza siku ile kwenye mkutano wa kijinsia, ndio huu. Mimi katu siwezi kujitesa hivyo mtoto wa kike. |
| **Baba Mamboleo:** | Kwa maneno hayo unataka kuniambia nini sasa! |
| **Mama** | Natakakukufahamishakuwahata |

**Mamboleo:** nilikotoka, mimi pia nina wazazi! Tusibabaishane! Sasa nakwambia nitachukua kiasi cha mzigo ninayoweza tu. Mingine nitaiacha. Mambo ni mbele kwa mbele! Hakunakubabaishanakamazamani enzi za ujima.

**Baba Mamboleo:** Ukiendelea kubishana na akina mamasaahiziutajikutaumeanzisha kesi nyingine. Ngoja nilale mbele!

**Mama Mamboleo:** Sisi akina mama tunaonekana ni punda tu wanaobebeshwa mizigo. Sijui akina baba wanataka waone magoti yameingia tumboni ndiyo waridhike? Hivi mtu kama mimi saa hizi muda wenye saa kumi, nikivunjika mgongo, itakuwaje? Lazimatukubalianekatikamaamuzi, na isitoshe kila jambo lina umuhimu wake. Hata akina mama siku hizi ni gharama na mali adimu bwana! Hakuna jambo la kiurahisi rahisi!

**Baba Mamboleo:**

(AnapoendeleamamaMamboleokuzungumzahivi, mumewe anaonekana akitokomea mbali na safari yake. Mara baada ya saa moja kupita baba

Matokeoaanarudinyumbaniakiwaamechangamka kiasi. Sasa endelea)

**Baba Mamboleo:** Eti we mwanamke! Ulichukua vifaa vyote nilivyokuwa nimekuagiza pale shambani au nawe unajaribu kutikisa kiberiti? Sasa nakuambia hivi, kama kuna kifaa ambacho umekiacha shambani, ni viganja na kipigo cha mbwa mwizi leo. Nataka kukuthibitishia, kuwa hujaolewa hapa kwa ajili ya kulea watoto tu. Hapa mama ni pamoja na kubeba mizigo mizito tunapotoka shambani. Na usipofanya hivyo ni fito na mkong'oto sawa? Isitoshe hata mila na jadi zetu zinakataa mwanaume kufanya kazi hizo! nisije nikachekwa wakadhani mimi ni tahira. Labda sana sana nikijisikia ndiyo naweza kukusaidia! Hivi wewe unafikiri lengo kubwa la kukulipia mahari ilikuwa nini? Ni kukufanyisha kazi kadri niwezavyo na isitoshe nikiona umeanza kuchakaa chakaa, nitafanya mabadiliko haraka ya kumsogeza bimdogo na kuchukua nafasi. Vipi hapo!

**Mama Mamboleo:** UsinishefueBabaMatokeo!Ina maanaumeninunuakamamfukowa plastiki?

| | |
|---|---|
| **Baba Mamboleo:** | Ndiyohivyo!Weweulifikiri nini? |
| **Mama Mamboleo:** | Jamani shida hizi zitakwisha lini kwetu wanawake?Kamakuolewakwenyewe ndiyo hivi!Basi tutaachika wengi,mimi nikiwa wa kwanza. |
| **Baba Mamboleo:** | We mwanamke umeshaniwekea maji ya kuoga au…? Mimi naona unahamu ya kupigwa, kwa sababu nimekudekeza sana wewe! |
| **Mama Mamboleo:** | Samahanimmewangunaletasasa hivi. |
| **Baba Mamboleo:** | Eti samahani mume wangu! Kumbe muda wote huo ulikuwa unanipigia kelele tu, haya harakisha |
| **Mama Mamboleo:** | Kwa kweli baba matokeo tabia hiyo ya kutothamini kazi za wengine, siyo siri inaniudhi sana. Dini…!! |
| **Baba Mamboleo:** | Hata kama umechukia kumbuka niliyezungumza ni mwanaume. Kwanza ujione una bahati ya namna ya pekee kunipata mwanaume kama mimi. Wenzio wanajitahidi kupepesa pepesa macho. Chunga!! Ngoja nikaogeusinipotezeemudawangu unanicheleweshakwenyekikao. |

*(MaratubaadayababaMamboleokutokakuoga mkewe akaanza kumuuliza pamoja na hasira alizokuwa nazo ilibidi acheke)*

| | |
|---|---|
| **Mama Mamboleo:** | BabaMamboleohiviunafahamu? |
| **Baba Mamboleo:** | Ah! Akina mama bwana! Kwa kweli kwa sababu ni ama zetu. Vinginevyo sijui…ehe haya sema! |
| **Mama Mamboleo:** | Nina wazo jinsi gani tuyaendeshe maisha yetu hapa nyumbani. |
| **Baba Mamboleo:** | Jamani oneni! Sasa!Huyu mwanamke anataka kunifundisha maisha. Uliona wapi yai likamfundisha kuku? Ngoja niwe na subira ehe! |
| **Mama Mamboleo:** | Unajua baba Mamboleo, naona umefika wakati muafaka wa kujadili na kufikia maamuzi ya pamoja katika masuala mbalimbali hapa nyumbani. Unaonaje juu ya wazo hilo Baba? |
| **Baba Mamboleo:** | Ukisikia Siku za kiama zimefika ndizo hizi! Hivi, toka lini, Mama akashirikishwa katika utoaji wa maamuzi ya aina yoyote ile? Siku zote toka enzi za mababu mwanamke yeye ni kufuata amri apende asipende, ajabuiposikumtasematugawane mapatosawa.MaraOh!Tunataka |

tumilikishwenyumba,ardhi,nyumba na rasilimali zote tunazomiliki sisi. Acha mawazo hayo siyo kila kitu ni cha kuiga.

**Mama Mamboleo:** Basi kwa taarifa yako ngoja nikupashe mambo yalivyo kabla hujaenda kwenye kikao ulichosema. Najua unasema kikao tu lakini unakokwenda kwani hakufahamiki? Sisi nani hii? Siku hizi mambo yamebadilika. Kuna mabadiliko ya mahusiano ya kijinsia ambayo husababishwa na hali ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia, kisiasa na kijiografia.

**Baba Mamboleo:** Ah! Na wewe mama matokeo una mbwembwe, mambo ya kijiografia yana mahusiano gani na mabadilikoya kijinsia. Eh! Unatakuja kuniambia nini?

**Mama Mamboleo:** Sikuhizikunamabadilikomengi.Kuna Sheria za kumiliki ardhi na mirathi zinazowatetea akina mama. Zaidi ya hayo zipo Sheria hata za haki sawa kwa watoto wote bila kujali kama ni mvulana au msichana. Isitoshe hata watoto ambao ni walemavu nao wana haki zao zinazowalinda kisheria. Kalaga baho!

**Baba** Ngojasasanikaekwanzakwakuwa

**Mamboleo:** hata tumbo limeshanivurugika. Mama Mamboleo kama mambo yenyewe unavyosema ni ya kweli, basi nakwambia sisi wanaume wameshatutengua. Kwisha kazi!

**Mama Mamboleo:** He, he, hee!!! Ya kisasa hayo!! Ngoja nikuongezee tena. Kwa taratibu za siku hizi hata zile mila kandamizi marufuku!Mlizoeamnokutunyanyasa.
Akina mama tu, ndiyo wamekuwa watu wa kupigwa, kubakwa, kukeketwa na tena hakuna hata mgawanyo mzuri wa mapato kati ya wanaume na wanawake. Siyo siri tumechoka.

**Baba Mamboleo:** Yaani haya yote uliyonieleza yangekuwa ni ya kweli, naona mgetukalia sana nyie wanawake. Lakini nafahamu ulinichenga tu! Ulijua nitakapokuwa ninatoka kuoga, labda sijakuulizia juu ya vifaa vyote kama umevirudisha hapa toka shambani. Kwa kawaida huwa sisahau mimi. Ngoja nikavae nguo kwanza halafu nije.

**Mama Mamboleo:** He, He, Heeeee!!! Maneno hayo mpaka tutakapofikia muafaka. Nikuelezebasiwenziosikuhizi wanakubalikubadilika.

| | |
|---|---|
| **Baba Mamboleo:** | Sikatai lakini siyo baba Mamboleo. Siwezi kubadilika katu. Subirini akina matokeo!! Mimi ni kisiki cha mpingo bwana ulizia uambiwe! |
| **Mama Mamboleo:** | He, he,he Heeee!!! Utabadilika tu ndiyo maana nakupenda, wewe mwepesi kweli kuelewa. |
| **Baba Mamboleo:** | MamaMamboleotafadhali!!!! |
| **Mama Mamboleo:** | Basi baba Mamboleo, kwa nini usikae kitako japo kidogo tu, usinikilize, vizuri na kuona kuna jambo gani muhimu ninalotaka kukueleza. Nakuomba uvute subira. |
| **Baba Mamboleo:** | Ni kweli unalosema! Labda isiwe kila naloambiwa nalifanyia mzaha. Mh! kwa kweli siku hizi! Yapo mabadiliko ambayo jamii inatakiwa kuyatazama kwa kina, tena kwa uangalifu. Hata hivyongojanikiruditutazungumza Zaidi!!. |

## (vii) Moderesheni

Moderesheni ni ujuzi ambao ni muhimu kwa mwezeshaji wa mjadala katika jamii ili kupata matokeo tarajiwa. Kuna tofauti kati ya mwenyekiti wa kikao au mkutano na mwezeshaji wa mijadala katika jamii.Mwenyekitihuwaongozawatukutoamaamuzi

na maazimio ya jambo linalojadiliwa na wakishindwa kukubaliana yeye ana kura ya veto ya kuwaamulia. Kwa upande mwingine mwezeshaji anawezesha mazingira ya washiriki kujadili kwa uhuru na kutoa maoni yao na wanaweza kutofautiana namwezeshaji huwafanya washiriki wa mjadala kutoa maoni yao ikiwepo na ukweli kuhusu jambo linalojadiliwa na hatimaye kutatua changamoto zinazowakabili.

**Namna ya Kutumia Moderesheni katika Kuwezesha Majadiliano**

Mwezeshaji utakapokuwa unawezesha majadiliano kwenye jamii kwa kutumia mojawapo wa mbinu au zana (i) hadi (vi) Unatakiwa uwe na:-uwezo wa kuzikiliza, kurudia misemo na mapendekezo yanayosemwa,na kuwezesha wajumbe wote kushiriki katika maamuzi. Ili kufanya hivyo inabidi washiriki wakuone hufungamani na upande wowote wakati wanapotofautiana kati yao.

**WakatiwaKutumiaModeresheni**

Modereshenihutumikakatikamazingirayafuatayo:-

(i) Wakati kuna haja ya kupata habari zaidi kuhusu kitu maalum

(ii) Wakati wa kuwezesha mikutano ya ushirikishwaji

**Muhimu**:- Katika mikutano baadhi ya washiriki wana aibu ya kuchangia mawazo yao. Kwa mbinu ya moderesheniwajumbewatakuwatayarikuchangia

kwa uhuru na itazuia baadhi ya wajumbe kumiliki majadiliano.

**Zana/Mbinuza Moderesheni**

Mbinu za moderesheni ni pamoja na:- kusikiliza, ukasuku, kudaka mpira, utoaji wa mhutasari na kutofungamana na upande wowote.

(a) **Kusikiliza:-**mtu anayetumia mbinu ya moderesheni atakiwa kuwa msikilizaji mzuri. Ni kwamba mtu awe na uwezo wa kuelewa nini hasa washiriki wanamaanisha katika misemo yao au matumizi ya viungo vya miili yao wakati wakiwa katika mikutano au majadiliano. Mwezeshaji anatakiwa kuwa na mdomo mdogo, masikio mapana yanayosikiliza sana.

(b) **Tumia mbinu ya Ukasuku**:- jambo ambalo limesemwa na mshiriki mmoja hurudiwa na mwezeshaji ili kuhakikisha kuwa:-

- Kila mshiriki katika majadiliano ameelewa lililozungumzwa na mshiriki mwingine.
- Msemaji anaweza kukiri kama usemi uliorudiwa unaonyesha kile kilichokusudiwa.

Mfano mshiriki wa majadiliano anasema *“nina wasiwasi na utendaji wa kamati yetu ya MTAKUWWA ya kiiji/mtaa”* wewe unarudia kwa kusema” *kwa hiyo una wasiwasi na utendaji wa kamati yenu ya MTAKUWWA ya kijiji/mtaa*”.

(c) **Tumia mbinu ya kudaka mpira**:- mbinu hii hutumika pale ambapo washiriki wa majadiliano wanaposhindwa kujadili jambo kwa uwazi ambalo unafikiri ndilo muhimu zaidi. Katika hali hii mwezeshaji unaweza kusaidia kwa kudaka misemo na maneno muhimu kutoka kwa washiriki ambayo yatasaidia kuleta majadiliano kulingana na ajenda, kufafanua na kumaliza kutoelewana.

Mfano mshiriki anasema "*ukeketaji wa watoto wa kike unazidi kuongezeka".* Mwezeshaji anadaka kwa kusema "*kwa hiyo, vitendo vya ukeketaji wa watoto wa kike vinazidi kuongezeka?"*

(d) **Kutoa mhutasari**:- mwezeshaji anapaswa kuwa na uwezo wa kutoa mhutasari wa kile kinachosemwa au kujadiliwa na washiriki wa majadiliano. Kwa kufanya mhutasari muafakawa misemo iliyotolewa na wajumbe mbalimbali na kudokeza hitimisho.

(e) **Kutofungamana na upande wowote**:- Mwezeshaji anayetumia moderesheni hana budi kuchukua tahadhari ya kutokuwa upande wowote ule au kuunga mkono mshiriki yeyote wakati wa majadiliano. Mtu anayetumia moderesheni hapaswi kutoa maoni yoyote au mawazo katika suala linalojadiliwa.

**Mpangokazi shirikishi**

Baada ya kufanya mjadala kwenye vikundi, kila kikundi kiteuwe wajumbe wawili watakaoshiriki kwenye timu ya kuandaa mpango kazi wa kushughulikia changamoto za Mila na Desturi. Timu ya mpango itahusisha na wajumbe wa Kamati ya MTAKUWWA ya kijiji/mtaa.

Mpango kazi utakaoandaliwa uoneshe malengo mahsusi, fursa, vikwazo, sababisho, ufumbuzi, hatua ya utekelezaji, mahitaji na gharama na viashiria.

**JedwaliNa.1:MpangoShirikishi**

| Malengo Mahsusi | Furasa | Vikwazo | Sababisho | Ufumbuzi | Hatua ya Utekelezaji | Mahitaji | Gharana | | Viashiria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Ndani | Nje | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

MpangoutakaoandaliwaukikamilikauwasilishwekwenyemkutanowahadharawaKijiji/Mtaa kwa ajili ya utekelezaji.

# SURAYA TANO

# UFUATILIAJINATATHMINISHIRIKISHI

Ufuatiliaji na tathmini shirikishi unapima mpango shirikishi wa kutatua changamoto za mila na desturi zinazochangia ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Kwa upande mwingine ni zile Mila na Desturi chanya zinazopaswa kuendelezwa na kutathmini matokeo yake katika kutomeza ukatili. Mapungufu yanayotokana na utekelezaji wa mpango yanaweza kutumika kurekebisha mpango kwa kuzingatia uzoefu na maarifa yaliyopatikana.

## UfuatiliajiShirikishi

Ufuatiliaji shirikishi wa utekelezaji wa mpango utapitia hatua zifuatazo:-

### Hatuaya1:Maandalizi

Wawezeshaji ngazi ya jamii watakutana na Viongozi ngazi ya jamii na wajumbe wa kamati ya MTAKUWWA ya kijiji/mtaa kwa ajili ya kukubaliana utaratibu wa ufuatiliaji na kuandaa ratiba ya utekelezaji wa mpango kazi.

### Hatuaya 2: UkusanyajiwaTaarifa/Takwimu

Wawezeshaji jamii watawezesha viongozi wa jamii na wajumbe wa kamati ya MTAKUWWA kukusanya taarifa/takwimu ili kuchambua utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kufanyika. Katika hatua hii watashirikiana:-

(i) Kuthibitisha taarifa/takwimu kwa kutembelea maeneo;

(ii) Kufanya majadiliano na watu wenye uelewa na mila na desturi; na

(iii) KupatatAarifazaMTAKUWWA.

**Hatuaya 3: UchambuziwaTaarifa/Takwimu**

Sehemu hii itahusisha uchambuzi wa taarifa na takwimu za kupima manafanikio yanayotokana na utekelezaji wa Mpango.

**HatuayaNne:KuwekaKumbukumbunaKutoaTaarifa**

Katika hatua hii wawezeshaji na viongozi wa jamiikwa kushirikiana na Kamati ya MTAKUWWA ya kijiji/mtaa wataandaa taarifa.

**HatuayaTano:MatumiziyaMatokeo yaUfuatiliaji**

Matumizi ya matokeo ya ufuatiliaji shirikishi yatumike katika mapitio na marekebisho ya Mpango.

**TathminiShirikishi**

Ni utaratibu wa kupima na kuchambua utekelezaji wa mpango kwa lengo la kupata taarifa zinazowezesha kufanya maboresho ya utendaji. Ni mchakato wa kupima utekelezaji wa malengo, matokeo ya programu ambapo kupitia tathmini mrejesho wenye funzo ndani yake hupatikana na hivyo husaidia kutoa ushauri stahiki unaosaidia kuboresha utendaji.

Chagua zana zinazofaa za kukusanya taarifa, kama vile, madodoso, mahojiano, mijadala ya vikundi lengwa na rejista ya washiriki.

### UmuhimuwaKufanyaTathmini

Katika muda wa kati hadi mrefu, tathmini zinaweza kuwa muhimu katika kupima:-

i. Hali ya utekelezaji wa mpango kazi kwa kupima ufanisi wa hatua za utekelezaji;
ii. Ufanisi wa majadiliano ngazi ya jamii kwa kuzingatia matarajio ya jamii na matokeo ya muda mrefu (Kuchunguza mabadiliko katika utendaji);
iii. Mbinu za utendaji - iwapo kuna mabadiliko katika maarifa, mtazamo, imani na desturi, kwa mfano, mabadiliko ya Mila na Desturi katika jamii zinazotoa fursa sawa kwa wanawake na wasichana kushiriki katika kufanya maamuzi ndani ya kaya na jamii;
iv. Kufanyamaamuzisahihi; na
v. Kama afua ni endelevu. Baada ya tathmini maamuzi ya afua zipi ni endelevu na zipi ziongeze hufanyika.

### Hatuaza TathminiShirikishi

Tathmini shirikishi ya utekelezaji wa mpango itapitia hatua zifuatazo:-

**Hatuaya1: Maandalizi**

Wawezeshaji ngazi ya jamii watakutana na viongozi ngazi ya jamii na wajumbe wa kamati ya MTAKUWWA ya kijiji/mtaa kwa ajili kulezea umuhimu wa tathmini shirikishi.

**Hatuaya 2: UkusanyajiwaTaarifa/Takwimu**

Katika hatua hii wawezeshaji jamii watawezesha viongozi wa jamii na wajumbe wa kamati ya MTAKUWWA kukusanya taarifa/takwimu ili kuchambua utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kufanyika.

**Hatuaya 3: UchambuziwaTaarifa/Takwimu**

Sehemu hii itahusisha upimaji wa matokeo ya utekelezaji wa Mpango ili kubaini mafanikio na mapungufu yatakayojitokeza na kutoa ufumbuzi.

**HatuayaNne:KuwekaKumbukumbunaKutoaTaarifa**

Katika hatua hii wawezeshaji na viongozi wa jamiikwa kushirikiana na Kamati ya MTAKUWWA ya kijiji/mtaa wataandaa taarifa.

**Hatua ya Tano: Matumizi ya Matokeo ya Tathmini Shirikishi**

Matokeo ya tathmini shirikishi yatumike katika mapitio na marekebisho ya Mpango. Uaandaji na utekelezaji wa Mipango Shirikishi ya Jamii.

## Rejea

*Changing Social Norms and Values to Eliminate Violence Against Women and Children Through Gender Transformation in Tanzania: An Assessment of Theory and Practices, 2020.*

*Mpango wa Taifa ya Kutokomeza ukatili wa Wanawake na Watoto 2017/18 - 2022/23.*

*Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi Zenye Madhara kwa Jamii, 2022.*